Nuru ya Kiswahili, Juzuu 3(2), Desemba 2024: 1-23
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru32.0123

# Mdhihiriko wa Anthroposenia katika Riwaya za *Bustani ya Edeni* na *Vipuli vya Figo:* Misukumo ya Tamaa na Ulofa

**Antony Kago Waithiru**
**Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu cha Laikipia**
kagoantony3@gmail.com

## Ikisiri

Makala hii inahusu uchanganuzi wa namna anthroposenia inavyodhihirika katika riwaya mbili za Emmanuel Mbogo, *Bustani ya Edeni* na *Vipuli vya Figo*, kwa kujikita katika misukumo ya tamaa na ulofa. Kusudi la makala hii ni kujadili mchango wa binadamu katika kukuza anthroposenia kupitia tamaa na ulofa. Mtindo wa uchambuzi wa maandishi ya fasihi ulitumika katika ukusanyaji wa data. Ukusanyaji na uchanganuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Uhakikimazingira iliyoasisiwa na Glotfelty & Fromm (1996). Nguzo zilizoongoza uchanganuzi huu ni binadamu dhidi ya maumbile, uwezo, na maendeleo endelevu. Kisha, data ilidondolewa kutoka kwenye riwaya mbili teule na kuchanganuliwa kupitia njia ya upekuzi-changanuzi wa maudhui kwa kuongozwa na nguzo tatu za Nadharia ya Uhakikimazingira. Hatimaye, ilidhihirika kuwa athari za viwanda vya kemikali katika uharibifu wa mazingira pamoja na tamaa na ulofa ni mazao ya shughuli za kila siku za binadamu katika kupalilia anthroposenia ulimwenguni. Makala hii imeonesha jinsi mtunzi, Mbogo, anavyotumia fasihi kuonya kuhusu madhara ya binadamu kwa mazingira, huku akihimiza mabadiliko ya mielekeo, mawazo na matendo kwa lengo la kuyahifadhi mazingira. Matokeo ya makala hii yanatoa mchango muhimu katika masuala ya kimazingira na maadili ya kisasa pamoja na kudhihirisha nafasi ya riwaya ya Kiswahili katika kuelezea na kupinga changamoto za anthroposenia.

**Dhana za Msingi**: Anthroposenia, shughuli, tamaa na ulofa

## Utangulizi

Makala hii inajadili namna shughuli za kila siku za binadamu zinavyozalisha na kupalilia anthroposenia kupitia tamaa na ulofa. Makala inashikiliwa na dhana muhimu za *shughuli* na *anthroposenia*. Hivyo, ili kurahisisha uelewa wa mjadala wa makala hii, tutaanza kufafanua dhana hizi.

Anthroposenia hurejelea kipindi katika maisha ya binadamu ambapo huyaharibu mazingira yake mwenyewe. Dhana ya anthroposenia imefafanuliwa kama epoki inayokipambanua kipindi cha sasa ambacho, kwa kiwango kikubwa, kimeathiriwa na shughuli za mwanadamu (Glaser na wenzake, 2014; Clark, 2015; Angus, 2016; Moore, 2016; Butler, 2024; Economides, 2025). Tangu kipindi cha miaka ya 1800 kumekuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira unaozalisha tabianchi yenye madhara kiikolojia. Wanaeleza kuwa anthroposenia ni epoki ambalo linatumiwa kuelezea kipindi na muda wa hivi majuzi katika historia ya ulimwengu, ambapo kuna shughuli za kibinadamu ambazo zimeathiri kwa kiwango kikubwa mifumo ya ulimwengu ya hali ya anga na ya kiekolojia. Hivyo, dhana ya anthroposenia imerejelewa kama kipindi cha kijiolojia ulimwenguni (Steffen na wenzake, 2008; Davis, 2015; Moore, 2017a na 2017b; Wallenhorst & Wulf, 2023; Burdon, 2023; Economides, 2025). Wataalamu hawa wanaeleza kuwa anthroposenia inatokana na shughuli za binadamu.

Shughuli ni dhana inayorejelea jambo ambalo linamfanya mja atumie nguvu, juhudi au jitihada na akili yake ili kuitekeleza; kazi au dimba (BAKITA, 2015; TUKI, 2006 & 2013). Katika makala hii, istilahi hii ilirejelea jambo, tukio au hali ambayo hutendwa na binadamu. Matendo hayo ambayo hufanyika kwa kutumia nguvu, jitihada, na teknolojia

huhusisha kujitafutia riziki, burudani, amani, maendeleo, mahusiano mema, ukulima au kupunga upepo katika ufuo wa bahari au kando ya mto. Ni dhahiri kuwa shughuli hizi, hasa za kujiendeleza kiuchumi, ndizo zinazozalisha anthroposenia kila uchao. Uchumi ni nomino ambayo hurejelea mali iliyopatikana kutokana na amali za nchi au watu. Pia, hurejelea mfumo wa mapato na matumizi ya watu katika nchi au taaluma ya mapato na matumizi ya watu (TUKI, 2014; Ndalu na wengine, 2014; na Mdee na wengine, 2015). Ulofa nao hutokana na hali ambapo mtu mwenye kipato kidogo huishi kwa dhiki.

Anthroposenia ilitambulishwa na ukweli kuwa shughuli za binadamu zimepiku matokeo ya kiulimwengu katika kusukuma dunia kwenye janga la uharibifu wa hewa, upungufu na ukosefu wa mvua, mmomonyoko wa udongo, ufyekaji wa misitu, umwagaji ovyo wa taka zenye kemikali na mbinu hatari za ukulima (Steffen na wenzake, 2008; Davis, 2015; Moore, 2017a na 2017b; Wallenhorst & Wulf, 2023; Burdon, 2023; Economides, 2025). Hata hivyo, makala hii inaangazia anthroposenia katika msingi wa uharibifu wa kiekolojia ila si wa kijiolojia. Wataalamu kama vile Moore (2017b), Simon & Mark (2018), na Coughlin na Gephart (2020) wanashikilia msimamo kuwa kando na binadamu kuchangia upujufu wa mazingira kijumla—anthroposenia—upujufu huu umechangiwa pakubwa na mataifa tajiri yenye uwezo.

Mathalani, Mbogo anadhihirisha namna wawekezaji kutoka mataifa tajiri huwekeza viwanda vya kemikali barani Afrika, huku wakivunja kanuni zote za Shirika la Afya Ulimwenguni za kulinda wafanyakazi na mazingira. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo na ile ya maendeleo endelevu. Moore (2017a) anasisitiza kuwa anthroposenia ni kipindi kinachotawaliwa na

shughuli za kila siku za binadamu ambacho huakisiwa kupitia njia mbili kuu. Njia ya kwanza ni ile ya mabadiliko makubwa duniani ambayo kando na kuashiriwa na ishara mahsusi za kizistografia katika mkabala wa kijiolojia. Hii huashiria vipindi tofauti vya mabadiliko ya kihistoria ya dunia kiuyakinifu—anthroposenia ya kijiolojia (Moore, 2017b; Ellis, 2018; Wallenhorst & Wulf, 2023; Butler, 2024; Chandler & Chipato, 2024; Economides, 2025). Shughuli kuu ambayo ilizalisha mabadiliko haya ni majaribio ya kinyuklia katika kipindi cha kati ya 1945 hadi 1960 kimwavuli.

Njia ya pili ni pale ambapo mataifa yaliyotawaliwa na mkoloni yalishuhudia kuhamishwa kwa Waafrika lukuki kama watumwa. Hili lilisababisha sio tu mauaji ya watumwa, bali pia uharibifu wa maeneo waliyoyatawala (Iheka, 2015), hususani barani Afrika, bila kujali athari zake hasi za kudumu dhidi ya wenyeji na viumbe vilivyomo (Moore, 2016; na Wallenhorst & Wulf, 2023). Tofauti na Moore anayeshikilia kuwa njia hii ya pili ni kapitalosenia (na si anthroposenia), makala hii yanashikilia msimamo kuwa hii ni anthroposenia na ni zao la binadamu kutokana na tamaa na ulofa. Ingawa tamaa na ulofa hudhihirika katika viwango na janibu tofauti ulimwenguni kijumla, katika makala hii, visababishi hivi viliangaziwa katika misingi ya fasihi katika riwaya mbili za *Bustani ya Edeni* na *Vipuli vya Figo*.

Wataalamu wengi katika taaluma ya anthroposenia wanakubaliana kuwa anthroposenia ni kipindi katika maisha ya binadamu kinachotawaliwa na shughuli za binadamu zinazohusiana na mahitaji, haja na mielekeo ya kimazingira (Demos, 2017; Ellis, 2018; DeLoughrey, 2019; Doherty, 2022; Wallenhorst & Wulf, 2023 & Butler, 2024). Michango ya wataalamu wa

hapo kabla kuhusu anthroposenia, hususani katika muktadha wa fasihi na mazingira, ilikuwa muhimu ingawa ulidhihirika mwanya ulioibua haja ya makala hii. Wataalamu kama Howarth (1995), Garrard (2004), Clark (2015) pamoja na Moore (2015, 2016) wanaangazia nguvu za fasihi katika kuelezea madhara ya binadamu kwa mazingira. Hata hivyo, kazi zao zimejikita zaidi katika fasihi za kimagharibi, huku fasihi za Kiafrika—hasa ya Kiswahili—zimeepukwa katika mijadala hii. Mathalani, masuala ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira yanayopata msukumo kutokana na tamaa na ulofa, ambayo yanaakisiwa na mwandishi Mbogo katika *Bustani* na *Vipuli*, hayajachunguzwa kwa kina. Kwa msingi huu, makala hii inanuia kujadili kujadili mchango wa binadamu katika kukuza anthroposenia kupitia tamaa na ulofa. Isitoshe, inanuia kupanua mjadala wa kitaaluma kwa kudhihirisha riwaya ya Kiswahili inavyoweza kuwa chombo madhubuti cha kuhamasisha mabadiliko ya kijamii na kimazingira.

Ingawa kwa jumla anthroposenia ni zao la shughuli za kila siku za binadamu, tamaa na ulofa ni mambo makuu yanayochangia ukuaji wa anthroposenia (Huggan & Tiffin, 2010; Waithiru na wenzake, 2024). Katika uchanganuzi wa makala hii, ilibainika wazi kuwa binadamu hufanikisha jukumu lake kama aina ya anthroposenia kupitia shughuli za kiuchumi pamoja na hulka yake ya kupalilia ulofa katika jamii. Hili lilidhihirika baada ya makala hii kuangazia mchango wa binadamu katika kupalilia anthroposenia kupitia tamaa na ulofa katika riwaya za *Bustani ya Edeni* (2002) na *Vipuli vya Figo* (1996). Makala hii itawapatia watafiti wa baadaye msingi wa kuchunguza riwaya ya Kiswahili kwa mtazamo wa uhakiki-mazingira. Wanajamii nao wanahimizwa kuwajibikia mazingira kwa kuyatunza na kuyahifadhi kwa kuzingatia mafunzo yanayotokana na

riwaya za *Bustani ya Edeni* na *Vipuli vya Figo.* Hatimaye, makala hii inatoa mchango muhimu katika kukuza mijadala ya kitaaluma na kijamii kupitia riwaya uchanganuzi wa riwaya za *Bustani ya Edeni* na *Vipuli vya Figo*.

**Maelezo Mafupi kuhusu Riwaya Teule**

Sehemu hii inatoa maelezo mafupi kuhusu riwaya mbili ambamo data zilizotumika katika makala hii zilikusanywa. Riwaya hizo ni *Bustani ya Edeni* na *Vipuli vya Figo* za Emmanuel Mbogo.

**Riwaya ya *Bustani ya Edeni***

Riwaya hii inajadili namna mazingira ya jana, leo na kesho yanavyonajisiwa na binadamu katika mfumo wa anthroposenia. Unajisi huu unadhihirishwa kupitia shughuli zinazoendelezwa ndani na nje ya kiwanda cha kemikali cha Siza. Bwana Abdula anajenga kiwanda cha *Saga Saga Chemical Industry* kinachozalisha madhara kwa wafanyakazi, wenyeji wa Siza na mazingira kwa jumla. Madhara ya uchafuzi wa mazingira yanasababisha ugonjwa wa 'Franco', nyasi kukauka na hewa kuchafuliwa. Ugonjwa huu unawafanya wenyeji wa Siza kuchubuka ngozi, vichwa kuwanga, miti kukauka, na mvua ya asidi. Pasta Yona wa Yona, kwa ushirikiano na wahusika wengine kama vile Jonalisti, Doricas, na Pamela wanajitoa mhanga kupigana na anthroposenia kwa hali, mali na uhai. Ingawa wahusika hawa wanaangamia katika vita vya kutetea uhifadhi wa mazingira, hatimaye, kiwanda cha *Saga Saga Chemical Industry* kinafungwa. Kisha, Bwana Abdula na familia yake wanarudi kwao Marekani.

**Riwaya ya *Vipuli vya Figo***

Riwaya hii inaelezea hali ya maisha ya Dkt. Matoga anapokuwa Waziri wa Afya na hatma yake baada ya kuondoka katika madaraka na kuendeleza kliniki yake ya *Mtoni Clinic*. Anaondolewa mamlakani baada ya kuhusishwa na kesi ya ufisadi. Baada ya kuondolewa ufahari huo, anajiingiza kwenye biashara ya vipuli vya figo. Mbogo amesawiri uhalisi wa anthroposenia ulimwenguni kupitia tamaa ya Dkt. Matoga, Profesa Williams na Dkt. Charles. Farihisi katika riwaya hii inasadifu maisha ya jamii pamoja na masuala yanayoizingira jamii hiyo. Dkt. Matoga pamoja na wafanyakazi wake watatu—Shipe, Nyau na Kipanga—wanadhihirisha unyama alionao binadamu. Wanalisafisha Jiji la Daluta kutokana na viwete, vipofu, vilema, vichaa, makahaba na maskini. Baada ya kuwaangamiza, wanawadondoa vipuli vya figo na mioyo, hatimaye, Dkt. Matoga, kwa ushirikiano na Profesa Williams na Dkt. Charles, wanaviuza Ughaibuni. Mwandishi amedhihirisha madhara ya anthroposenia kwa mwanadamu na mazingira yake kupitia uovu na uozo wa jamii kwa jumla.

**Msingi wa Nadharia**

Makala hii inaongozwa na baadhi ya nguzo kuu za Nadharia ya Uhakikimazingira. Nadharia hii iliasisiwa na Glotfelty & Fromm (1996). Glotfelty na Fromm wanashikilia msimamo kuwa Nadharia ya Uhakikimazingira huchangia pakubwa katika uhakiki wa matini za fasihi kwa kujikita kwenye vyambajengo vya ugiligili, uhusiano na uathirianaji baina ya binadamu na mazingira anamoishi au yanayomzingira. Quick (2004), Garrard (2007), Adamson & Monani (2020), Waithiru (2022a na 2022b), Garrard (2023) na Waithiru na wenzake (2023) wanafafanua kuwa uhakiki wa kimazingira hupambanua mikabala, mielekeo na maoni

mbalimbali ya namna fasihi ya kimazingira huangazia changamoto zinazoyakabili mazingira kila uchao katika mfumo wa anthroposenia. Nguzo zilizoongoza uchunguzi uliozalisha makala hii ni binadamu dhidi ya maumbile, uwezo, na maendeleo endelevu. Clark (2015), Iheka (2015), Davis & Turpin (2015), Butler (2024) na Burdon & Martel (2025) wanasisitiza kuwa, kuna haja ya kushughulikia anthroposenia katika misingi ya kiuhakikimazingira, kwa kuwa anthroposenia isipotatuliwa ina uwezo wa kumwangamiza binadamu pamoja na mazingira yake kimwavuli.

## Methodolojia

Makala hii ni zao la utafiti wa maktabani. Riwaya mbili za Emmanuel Mbogo zilisomwa kwa kina. Mkabala wa makala uliotumiwa ni wa kimaelezo ambao hujihusisha na kuchanganua suala la utafiti pasipo na kubadilisha vibadala (Yin, 2014). Ukusanyaji wa data ulihusisha uchambuzi wa maandishi ya fasihi katika riwaya za *Bustani ya Edeni* na *Vipuli vya Figo*. Njia kuu ya uchanganuzi wa data ilikuwa mbinu ya upekuzi-changanuzi wa maudhui. Uchanganuzi wa data ulihusisha mbinu ya kithamani kwa kuwa wenyewe ulijishughulisha na utafiti wa kithamani ila si wa kiwingi-idadi. Riwaya za *Bustani ya Edeni* na *Vipuli Vya Figo* ziliteuliwa kwa kudhamiria kutokana na kusheheni masuala chungu nzima kuhusu anthroposenia. Mvumbi & Ngumbi (2015) wanasisitiza kuwa sampuli matilaba huweza kuwa muhimu sana katika hali ambapo suala la msingi kwa mtafiti ni kufikia sampuli lengwa kwa wepesi na upesi.

## Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya mjadala kuhusu jinsi misukumo ya tamaa na ulofa inavyochangia anthroposenia katika riwaya mbili teule mintarafu ya lengo la makala. Palidhihirika muumano kati ya nadharia ya

Uhakikimazingira, mbinu za utafiti na uhusiano kati ya data na lengo la makala. Riwaya za *Bustani ya Edeni* na *Vipuli vya Figo* zimeonesha namna uharibifu wa mazingira unasababishwa na shughuli za binadamu. Hili lilifanikishwa kupitia mjadala kuhusu namna wahusika na matukio katika riwaya mbili teule yanavyoakisi tamaa na ulofa kama vichocheo vya uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Mbogo amefanikiwa kudhihirisha namna matendo ya binadamu yanavyoongozwa na uchoyo na tamaa. Matendo haya yanaathiri mazingira kwa njia hasi. Riwaya hizi mbili teule zina mchango mkubwa katika kuelewa changamoto za anthroposenia na kuhamasisha jamii kuhusu haja ya mabadiliko ya tabia za kimazingira, hali ya hewa na misimu kwa ujumla. Makala hii yanajumuisha uchambuzi wa kina, uhusiano wa Nadharia ya Uhakikimazingira katika kazi za kifasihi pamoja na umuhimu wa fasihi katika kushughulikia changamoto za anthroposenia.

**Athari za viwanda vya kemikali**

Viwanda vya kemikali katika riwaya za *Bustani* na *Vipuli* vilidhihirika kuwa na uwezo mkubwa wa kuyaharibu mazingira zaidi ikilinganishwa na uwezo wao wa kuyahifadhi mazingira. Mwandishi ameonesha namna tamaa na ulofa huchangia ujenzi wa viwanda vya kemikali na matokeo yake huwa uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Hili linawiana na kauli ya Waithiru (2022b) kuwa viwanda vya kemikali kama haja ya kuendeleza maendeleo endelevu husababisha madhara dhidi ya binadamu na mazingira yake kwa jumla (Waithiru, 2022b). Mathalani, kupitia mhusika Doricas katika riwaya ya *Bustani ya Edeni*, inadhihirika kuwa uchafuzi wa mazingira husababisha njaa. Doricas akiwa na wasiwasi anampa mwanawe, Samsoni, ziwa ambalo limechokachoka kwa kukosa maziwa ya kutosha. Ingawa Samsoni analinyonya, njaa inaendelea kumsakama, madhali ziwa la mamake lina

maziwa kidogo mno. Binadamu katika harakati zake za kujiendeleza kiuchumi, anajenga viwanda ambavyo vinachangia anthroposenia pakubwa. Kwa mfano, kiwanda cha kemikali cha *Saga Saga Chemical Industry* kinachangia upungufu wa hewa kwa kiwango kikubwa pale eneo la Siza. Hili linadhihirishwa na Doricas anapopiga chafya mfululizo kutokana na maradhi yanayosababishwa na hewa chafu. Analalamika kuhusu mwasho unaotawala pua zake kila anapopiga chafya hadi inambidi atumbukize kidole ndani ya matundu ya pua, moja baada ya lingine, kuyachokonoachokonoa, mradi apunguze mwasho na mnyegeo unaomnyima amani na utulivu.

Shughuli za binadamu za kujiendeleza kiuchumi zimechangia kunawiri kwa anthroposenia. Hii ni kwa sababu matokeo yake ambayo ni hatari kwa viumbe hai yanaendelea kuenea ulimwenguni. Davis (2015), Davis & Turpin (2015) na Waithiru (2019) wanafafanua kuwa shughuli na juhudi za binadamu za kujiendeleza, kama vile uundaji wa plastiki, zinaendelea kuimarisha anthroposenia kwa kuzorotesha afya ya binadamu, na kualika kifo kwa haraka. Mbogo, akishadidia ukweli huu katika riwaya ya *Bustani ya Edeni*, anamtumia mhusika Eliya kudhihirisha athari hasi za anthroposenia kama zao la juhudi na jitihada za binadamu, hususani za matajiri na viongozi. Eliya, mumewe Doricas, alikuwa amekumbwa na kikohozi kisichokwisha pamoja na ugonjwa wa kuwasha ngozi. Maradhi haya yalikuwa yameenea katika janibu za Siza kutokana na kemikali zilizozalishwa na kiwanda cha *Saga Saga Chemical Industry*. Walioathirika zaidi, kando na wenyeji wa Siza, ni wafanyakazi katika kiwanda kile. Hakika, shughuli hizi za kujiendeleza kiuchumi huchangia uchafuzi wa mazingira kwa kiasi kikubwa. Hali hii inawiana na kauli ya akina Clark

(2015) na Moore (2016) kuwa maradhi mengi anayayoyaasisi mwanadamu yanachangia kifo chake kiafya, kiuchumi na kimazingira kwa haraka sana.

Katika anthroposenia, binadamu amejiathiri mwenyewe kwa njia hasi sana. Mathalani, Samsoni anamweleza Doricas kuwa kiwanda kile kiliwaathiri wakazi wote wa eneo la Siza. Samsoni anakiri kuwa kila mtu ama anakohoa au anajikuna ngozi. Ilifikia kiwango kwamba wenyeji walitania na kuurejelea kama ugonjwa wa kupiga gita ama Franco. Doricas anaongeza kuwa, hata nywele zinanyonyoka na vichwa kushamiri vidonda kama kile cha Baba Mohamed. Hapa, Doricas anadhihirisha kuwa binadamu anajiponza mwenyewe pamoja na kizazi chake katika anthroposenia. Mathalani, katika *Bustani ya Edeni* Doricas anamlaani mende kuwa: "... Shenzi!" Kwa kasi, alimpiga kofi mende mwingine tena aliyekuwa anacheza na kuking'ong'osa kidonda cha mwanawe kichwani." (uk. 10).
Hili linadhihirisha kuwa binadamu anajisababishia maradhi na maangamizi.

Kadhalika, anapojiendeleza kiuchumi, vitendo vya binadamu—vinavyoongozwa na tamaa ya utajiri, ubinafsi, uchoyo na unajisi dhidi ya mazingira—vimechangia kuendeleza anthroposenia, na hivyo vimehatarisha uhai wa viumbe vyote (Walder, 2011 na Waithiru, 2022b). Mathalani, Mbogo anafafanua kuwa Mto Zamala ulikuwa umepungua sana Samaki, tofauti na kitambo ambapo walikuwa wengi. Upungufu huu umezalishwa na Kiwanda cha Saga Saga. Takataka na mafutamafuta ya kiwanda hiki yalielekezwa ndani ya Mto Zamala. Kutokana na sumu ya takataka na mafutamafuta, maisha ya viumbe na mimea yaliweza kuhatarishwa kwa kiasi kikubwa. Hali hii inafungamana na nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile. Ukiukaji wake wa kanuni za mazingira katika mtagusano wake na mazingira yake unasababisha anthroposenia. Binadamu, baada ya

kuimeza sumu kupitia maji au samaki, huweza kupatwa na maradhi; hatimaye huweza kuangamia. Mimea nayo huweza kukauka na kuvisababishia viumbe hai njaa ambayo inaweza kusababisha maafa.

**Tamaa na ulofa kama chanzo cha anthroposenia**

Kupitia tamaa na ulofa, mwandishi anadhihirisha namna binadamu huendeleza anthroposenia katika harakati za kujitajirisha na kujitawala kiuchumi. Hali hii inafungamana na nguzo ya maendeleo endelevu. Kwa mfano, mwandishi Mbogo katika riwaya ya *Vipuli vya Figo* anamsawiri Profesa Williams kama aina ya anthroposenia. Profesa Williams ni daktari maarufu sana Ughaibuni. Anaashiria anthroposenia kupitia shughuli zake za kila siku. Kama fundi mwingine yeyote ambaye hukarabati vifaa, mahali au vitu mbalimbali, Profesa Williams anatafuta vipuli vya figo na mioyo duniani kote ili kuvipachika kwa wagonjwa wake ambao wanamlipa pesa taslimu. Wagonjwa wake wengi walikuwa wameathirika na anthroposenia na kuugua maradhi mbalimbali. Maradhi haya yasiyokuwa na tiba yanaathiri figo au mioyo yao. Hivyo, Profesa Williams anapalilia anthroposenia kwa kuvitumia viungo vya mwili vya wanyonge kama vifaa vya kumfaidisha kifedha na matajiri kwa mkupuo mmoja. Hili linafungamana na nguzo ya maendeleo endelevu. Kutokana na ulofa binadamu anaongozwa na tamaa katika kuyaharibu mazingira yake katika mfumo wa maonevu.

Mjomba wake Dkt. Matoga anasawiri aina ya anthroposenia kama binadamu. Kama Mkuu wa Magereza, anapalilia anthroposenia kwa kumshauri Dkt. Matoga kushiriki mradi wa vipuli vya binadamu, hususani figo na mioyo. Kulingana na Mdee na wengine (2015), BAKITA (2015) na TUKI (2013), figo ni kiungo kilicho ndani ya mwili wa binadamu au wa

mnyama au wa ndege, ambacho hufanya kazi ya kusafisha damu na kutoa uchafu mwilini. Wanaongeza kuwa moyo ni kiungo kilicho katika mwili wa viumbe hai kama vile binadamu au wanyama, ambacho husukuma damu na kuieneza mwilini kote. Suala la msingi linalodhihirika katika riwaya ya *Vipuli vya Figo* ni kuwa, kutokana na majukumu muhimu yanayotekelezwa na viungo hivi viwili—figo na moyo—mwilini, ukosefu au tatizo linalotokea katika viungo hivi huweza kusababisha kifo.

Hivyo, Mbogo kusawiri shughuli ya uwindaji na uuzaji wa vipuli vya figo na moyo kama anthroposenia ni suala lililohalisi na linalolandana na nguzo kuu za anthroposenia ambazo hulenga kuleta maangamizi ya kila aina na hali. Shughuli hii ni hatari na ndiyo sababu Mkuu wa Magereza anamshauri Dkt. Matoga na kumsisitizia haja ya kuweka siri kubwa kadiri iwezekanavyo ili afanikiwe. Kwa misingi hiihii, Banko—Bosi wa Bandari—amesawiriwa kama aina ya anthroposenia kutokana na hulka yake ya ufisadi unaopalilia biashara ya uuzaji wa vipuli vya figo na mioyo. Magamba pia amesawiri anthroposenia kuanzia asili yake hadi kazi, hulka na imani yake. Katika Jiji la Daluta, hamna aliyebaini hasa asili ya Magamba ingawa walichokijua wote ni kuwa hakuwa mwenye asili ya eneo lile. Hata hivyo, asili yake ni zao la anthroposenia ambalo ni utumwa. Hii ni kwa sababu, baba ya babu yake alifika jijini Daluta kama mtumwa katika enzi za biashara ya utumwa iliyokuwa imeshamiri kutokana na juhudi za Waarabu. Kwa misingi hii, Waarabu pia ni aina ya anthroposenia. Biashara ya utumwa ni baadhi ya mojawapo ya matokeo ya anthroposenia. Watson & Watson (2007) wanayakinisha mtazamo wetu kuwa asili ya anthroposenia ni ubaguzi na dhuluma zilizochipuka kama zao la biashara ya utumwa

ulimwenguni. Athari moja hasi ya anthroposenia ni ulofa uliokidhiri. Hili linadhihirishwa na urithi wa Magamba.

Dkt. Matoga alipokuwa mwanasiasa mwenye uwezo, mamlaka, na sauti hakuwajali wananchi. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo ya Nadharia ya Uhakikimazingira, madhali mataifa tajiri huyanyonya yale fukara raslimali na kisha kuyachafulia mazingira yake bila kujali matokeo yake. Dkt. Matoga akishikilia wadhifa wa Waziri wa Afya, anafuja pesa takribani milioni sitini za umma ilhali wagonjwa wanaaga dunia kutokana na ukosefu wa dawa hospitalini na zahanatini. Magamba anamkumbusha kuwa kijiji chao ni duni kutokana na kutelekezwa na serikali. Dkt. Matoga anahisi kuwa ukumbusho huu ni mwasho wa simango ndani ya moyo wake madhali alipokuwa mbunge na Waziri wa Afya na alihusika katika utunzi wa sera mbalimbali za maendeleo na sheria za kudhibiti utawala, hakuwajali wanyonge na sasa mkweche wake umezima baada ya kuingia shimoni kwenye barabara alizozitelekeza. Dkt. Matoga anapolalamika kuwa barabara za akina Magamba ni mbaya, Magamba katika *Vipuli vya Figo* anamjibu kuwa, "... serikali ndiyo imezisahau" (uk. 75).

Ili kudumisha anthroposenia, ufukara hutawala na kuwa kama vile koroboi inayotoa mwanga mlegevu na harufu ya moshi inayotamalaki kwenye kibanda cha Magamba. Magamba na Dkt. Matoga wanaendelea kusawiri anthroposenia wanapohimizana katika njama ya kuiba maiti kutoka mochware anakofanya kazi Magamba kama mhudumu. Baada ya zao la anthroposenia kwa binadamu ambalo ni kifo kutokana na athari hasi zao, Magamba na Dkt. Matoga wanaimarisha anthroposenia kwa kuvuna vipuli vya figo na mioyo kutoka kwa wafu na mizoga. Siri na kazi wanayoshirikiana ni taashira ya anthroposenia. Magamba anakiri kuwa ile

ni kazi inayobidi wawe na ujasiri na moyo wa kuitunza siri ya mauti. Dkt. Matoga anataja kuwa, "... siri hiyo ni maiti" (uk. 77). Kauli hii ya Dkt. Matoga inathibitisha kuwa anthroposenia yenyewe kupitia shughuli yao ya kiuchumi ni maiti na huzalisha mauti. Isitoshe, Magamba anaisawiri anthroposenia kupitia msaada wa maiti na viungo vya maiti anavyowapatia wachawi, waganga, wafanyabiashara, wanasiasa na viongozi tofauti tofauti. Sanaa ya sihiri na kiza anayoshiriki Magamba inaashiria anthroposenia yenyewe.

Nguzo kuu inayowaongoza Dkt. Matoga na Magamba kuipalilia anthroposenia ni pesa. Kwa misingi hii, pesa ni taashira ya anthroposenia. Dkt. Matoga anapokumbuka namna mradi wa vipuli vya figo na mioyo utakavyofungua mikoba ya hazina, woga unamkimbia, nguvu na ujasiri vinamvamia na anabadili sauti. Kwa ujasiri, anafafanua: "Nitahitaji maiti ... kila siku: wake, waume kwa watoto wa aina na sampuli zote" (uk. 78). Hili linathibitisha kuwa, ikizingatiwa kuwa wote wawili ni aina ya anthroposenia na shughuli yao ya kiuchumi inatawaliwa na maiti, hatima kuu ya anthroposenia ni maafa. Hata hivyo, maafa haya hutokana na athari hasi za anthroposenia dhidi ya binadamu. Dkt. Matoga anaweka hili wazi anapoeleza kuwa, watu wengi hufa kutokana na ajali, ujambazi au hata maradhi mengi ya kawaida kutokana na udhoofu wa huduma za afya. Hata Magamba mwenyewe anatishwa na mradi huu ambao umejaa mizungu na vizungumkuti asivyowahi kukumbana navyo na kijasho kinamtoka kwapani. Hili linadhihirisha kuwa anthroposenia hutisha hata wale wanaoipalilia na kuilinda. Hata hivyo, tamaa ya kutajirika, ubinafsi na uchoyo vinawapa Magamba na Dkt. Matoga ujasiri wa kuipalilia anthroposenia. Dkt. Matoga anapalilia anthroposenia kupitia ufisadi na

ubadhilifu wa mali ya umma anapomwambia Bruno kuwa awe mwangalifu katika kazi yake pale zahanatini ili asipate hasara. Anasisitiza kuwa ingekuwa wakati alipokuwa waziri, hangejali hasara kwa kuwa ingekwua hasara ya serikali (siyo yake), lakini kwa sasa Bruno awe makini ili pasitokee hasara yoyote. Kwa misingi hii ya uongozi mbaya, Mkuu wa Magereza anasawiriwa na mwandishi kama aina ya anthroposenia.

Kadhalika, Nyau, Kipanga na Shipe wanaashiria anthroposenia. Kando na wao kushirikiana na Dkt. Matoga katika mradi wa uwindaji, upasuaji na usafirishaji wa vipuli vya figo na mioyo, wanawaua viwete, maskini na wanawake wanaoshiriki umalaya usiku. Uaminifu na utu wao kwa jumla unanunuliwa na pesa. Mkuu wa Magereza anadhihirisha hili kwa kusema: "Tunategemea pesa kununua uaminifu wao" (uk. 103). Vilevile, anashirikiana na Dkt. Matoga kuiba viungo vya figo na mioyo kutoka kwa wafungwa wanaonyongwa. Anthroposenia hutumia woga kujiendeleza. Hili linathibitishwa na mwandishi anayemsawiri Dkt. Matoga kwa kusema: "… (Dkt. Matoga) alishusha sauti na kusema kwa woga ... "Wale wanaonyongwa." (uk. 104, ufafanuzi wa kwenye mabano ni wa mwandishi wa makala hii).

Rais Gorbachev pia anaashiria anthroposenia kupitia msimamo na mfumo wake wa kisiasa na kiuchumi wa kibepari na soko huru. Hili linawekwa bayana na Dkt. Matoga anayeweka furaha ya ndani kwa ndani baada ya kusoma maelezo kwenye gazeti la *Daily Echo* yaliyosema kuwa, Rais Gorbachev amerejeshwa madarakani baada ya waasi—viongozi wa Kirusi—wakomunisti kushindwa kumuondoa mamlakani, yeye na ubepari wake. Waasi hawa ni tishio kwa anthroposenia kupitia msimamo wao wa siasa ya ujamaa na itikadi za Kimaksi na Kilenini, kulingana na Mbogo.

Rais Gorbachev anapalilia anthroposenia kupitia mfumo wa uchumi wa kibeberu unaojikita kwenye mhimili wa ubaguzi. Dkt. Matoga anatetea ubepari kwa kusisitiza kuwa, ni mfumo mzuri kwa sababu hata malaika wote hawako sawa; majini pia yana daraja zao tofauti; binadamu nao wana matabaka na ubaguzi wa aina aina.

Anaendelea kuwalinganisha nyuki na ubepari kwa kusisitiza kuwa, mzingani mna nyuki ambao ni walinzi na ambao hukaa tu wakalishwa. Kadhalika, mna wenye hufanya kazi kwa bidii, wenye kufanya mahaba na malkia, na wenye kufanya vibarua kwa kuwatumia nyuki wenye hadhi. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo, ambapo wenye mamlaka na nguvu huwanyanyasa wanyonge. Dkt. Matoga anafaulisha kauli yake katika misingi ya dini na kukariri kuwa, "... hiyo hali kaiumba mungu. Sijui binadamu wanashindwaje kuelewa mambo haya ya kawaida" (uk. 108).
Katika *Bustani ya Edeni*, Balozi Suprano pia anasawiri aina ya anthroposenia. Anamkumbusha Dkt. Matoga kuwa, ikiwa alipokea vyombo vyote vya upasuaji na vya kuhifadhi vipuli, ahakikishe kuwa biashara yao iko shwari. Anatumia mamlaka yake kutoa kinga ya kibalozi ili kuifanikisha biashara hiyo. Anasema: "Nataka hii biashara iwe *fool proof* (yaani isijulikane na yeyote serikalini – tafsiri ya mtafiti)" (uk. 114).

Hili linadhihirisha kuwa Balozi Suprano anatumia mamlaka yake kuilinda na kuiendeleza anthroposenia mjini Daluta. Ikizingatiwa kwamba Balozi Suparano ni taashira ya viongozi wa mataifa tajiri ya Ughaibuni ilhali Dkt. Matoga ni taashira ya viongozi wa mataifa fukara ya Afrika, ni dhahiri kuwa viongozi wa mataifa tajiri ya Ughaibuni huikuza, huipalilia na huiimarisha anthroposenia katika mataifa fukara ya Afrika na kuyanufaisha mataifa na wananchi wao, huku wakiwatumia wananchi wa mataifa ya

Afrika kama vifaa au shashi ila sio kama binadamu. Hivyo, mataifa ya Afrika huendelea kufifia na kukaushwa na anthroposenia huku yale ya Ughaibuni yakifaidi na kunenepa kwa raha. Hali hii inalandana na nguzo ya uwezo.

**Hitimisho**

Makala hii imejadili namna tamaa na ulofa unavyoendeleza na kukuza anthroposenia hasa katika mataifa yanayoendelea kwa kuangaza riwaya mbili za Emmanuel Mbogo. Mjadala huu uliongozwa na nguzo za binadamu dhidi ya maumbile, uwezo na maendeleo endelevu za nadharia ya uhakikimazingira. Mwandishi huyu amefanikiwa kuwasilisha ujumbe lengwa kwa ufanisi kupitia mjadala kuhusu athari za viwanda vya kemikali katika janibu zinazoendelea duniani pamoja na tamaa na ulofa katika janibu mbalimbali. Tamaa imedhihirishwa kupitia ujenzi wa viwanda, uuzaji wa mafuta, mikopo ya kiutumwa, na uvunaji wa vipuli vya figo na mioyo kutoka kwa wanyonge, viwete, wafungwa, wagonjwa, na makahaba. Mbogo amedhihirisha kuwa ufukara na anthroposenia huwa na uhusiano wa kisimbiyotiki, ambapo hali zote mbili hutegemeana na kukamilishana.

Kadhalika, makala imedhihirisha namna viongozi wa mataifa yenye uwezo huwatumikisha wale wa mataifa duni, huku wakiyanajisi mazingira yao duni katika mfumo wa umiliki na utawala wa kibeberu. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo iliyokuwa mojayazo ya nguzo zilizoongoza uhakiki wa makala hii. Mbogo anasisitiza haja ya binadamu kukabiliana na anthroposenia katika ulingo wa kisanaa kwa lengo la kusikitikia mazingira kwa jumla. Ingawa kwa kiwango kikubwa mazingira yameachiwa nyanja za sayansi kuyashughulikia na kuyahifadhi, fasihi ina nafasi kubwa ya kuyaangazia mazingira kwa uketo. Hii ndiyo sababu

makala hii imejadili kuhusu mchango wa binadamu katika kuendeleza anthroposenia duniani kwa kujikita katika shughuli zake za kiuchumi ambazo hutawaliwa na tamaa na ulofa kwa kiwango kikubwa. Makala inatoa msingi wa kitaaluma kwa watafiti wa baadaye kuchunguza kazi zingine za kifasihi za Kiswahili kuangaza anthroposenia. Hivyo, makala hii inachangia kukuza uelewa wa kijamii na kielimu kuhusu changamoto za anthroposenia. Aidha, inatoa wito kwa watafiti wa baadaye kuendeleza mijadala ya kina kuhusu nafasi ya riwaya ya Kiswahili katika kushughulikia masuala ya mazingira na maendeleo endelevu.

**Marejeleo**

Adamson, J. na Monani, S. (Wah.). (2020). *Ecocriticism and Indigenous Studies Conversations from Earth to Cosmos* (Toleo la 1.). London: Routledge.

Angus, I. (2016). *Facing the Anthropocene*. New York: Monthly Review Press.

BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Burdon, P.D. (2024). *The Anthropocene New Trajectories in Law* (Toleo la 1.). London: Routledge.

Burdon, P.D. & Martel, J. (Wah.). (2025). *The Routledge Handbook of Law and the Anthropocene* (Toleo la 1). South Australia: Routledge.

Butler, R.D. (Mh.). (2024). *The Anthropocene* (Toleo la 1.). London: Routledge.

Chandler, D. & Chipato, F. (2024). *Race in the Anthropocene Coloniality, Disavowal and the Black Horizon* (Toleo la 1). London: Routledge.

Clark, T. (2015). *Ecocriticism on the Edge: The Anthropocene as a Threshold concept*. London: Bloomsbury Academic an Imprint of Bloomsbury Publishing PLC.

Coughlin, M. & Gephart, E. (2020). *Ecocriticism and the Anthropocene in Nineteenth – Century Art and Visual Culture*. New York, NY and London: Routledge Taylor & Francis Group.

Davis, H. (2015). "Life and Death in the Anthropocene: A Short history of Plastic." Katika Davis H. na Turpin E. (Wah.). *Art in the Anthropocene: Encounters AmongAesthetics, Politics, Environment and Epistemologies.* London: Open Humanities Press, kur. 347-358.

Davis, H. & Turpin, E. (Wah.). (2015). *Art in the Anthropocene Encounters Among Aesthetics, Politics, Environments and Epistemologies*. London: Open Humanities Press.

DeLoughrey, E. (2019). Towards a Critical Ocean Studies for the Anthropocene. *English Language Notes* 57(1), 21-36. Inapatikana katika https://www.muse.jhu.edu/article/724603. Ilisomwa tarehe 22 Aprili 2021.

Demos, T.J. (2017). *Against the Anthropocene: Visual Culture and Environment Today*. Berlin: Sternberg Press.

Doherty, P. (2022). Reading Children's Literature in the Anthropocene: The Representation of 'nature' in Ursula K. Le Guin's Earthsea Fiction. *Children's Literature in Education*, 55(2), 1-15. Inapatikana katika https://doi.org/10.1007/s10583-022-09490-z. Ilisomwa tarehe 3 Januari 2023.

Economides, L. (2025). *Wild Anthropocene Literature and Multispecies Justice in Deep Time* (Toleo la 1). Montana: Routledge.

Ellis, E.C. (2018). *Anthropocene A Very Short Introduction*. Oxford: Oxford University Press.

Garrard, G. (2004). *Ecocriticism*. London: Routledge.

Garrard, G. (2007). Ecocriticism and Education for Sustainability. *In Pedalogy: Critical Approaches to Teaching Literature, Language, Composition & Culture*, 7(3), 359-386.

Garrard, G. (2023). *Ecocriticism* (Toleo la 3). London: Routledge.

Glaser, M., Krause, G., Ratter, B.M.W. & Welp, M. (Wah.). (2014). *Human-Nature Interactions in the Anthropocene Potentials of Social-Ecological Systems Analysis* (Toleo la 1). New York: Routledge.

Glotfelty, C. na Fromm, H. (Wah.). (1996). *Ecocriticism Reader: Landmarks in Literary Ecology*. Athens na London: The University of Georgia Press.

Howarth, W. (1995). *Some Principle of Ecocriticism*. Georgia: University of Georgia.

Huggan, G. & Tiffin, H. (2010). *Postcolonial Ecocriticism: Literature, Animals, Environment*. London na New York, NY: Routledge.

Iheka, C.N. (2015). *African Literature and the Environment: A Study in Postcolonial Ecocriticism* (Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Michigan, Michigan.

Mbogo, E. (1996). *Vipuli Vya Figo*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbogo, E. (2002). *Bustani ya Edeni*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mdee, J.S., Njogu, K. na Shafi, A. (2015). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Moore, J.W. (2015). *Capitalism in the Web of Life*. London: Verso.

Moore, J.W. (2016). *Anthroposecene or Capitalocene? Nature, History, and the Crisis of Capitalism*. Oakland, CA: KAIROS PM Press.

Moore, J.W. (2017a). The Capitalocene, Part I: On the Nature and Origins of Our Ecological Crisis. *The Journal of Peasant Studies*, 44(3), 594-630. Inapatikana katika https://dx.doi.org/10.1080/03066150.2016.1235036. Ilisomwa tarehe 7 Mei 2020.

Moore, J.W. (2017b). The Capitalocene Part II: Accumulation by Appropriation and the Centrality of Unpaid Work/Energy. *The Journal of Peasant Studies*, 45(2), 237-279. Inapatikana katika

http://dx.doi.org/10.1080/03066150.2016.1272587. Ilisomwa 21 Juni 2020.

Mvumbi, F.N. & Ngumbi, E.K. (2015). *Companion to research methodology: focus on humanities, education and social science.* Nairobi: CU.

Ndalu, A.E., Babusa, H. & Mirikau, A.S. (2014). *Kamusi Teule ya Kiswahili: Kilele cha Lugha*. Nairobi: East African Publishers.

Quick, P.S. (2004). *An Ecocritical Approach to the Southern Novels of Cormac Mccarthy* (Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Georgia, Georgia.

Simon, L.L. & Mark, A.M. (2018). *The Human Planet How We Created the Anthropocene*. A Pelican Book: Penguine Books Publisher.

Steffen, W., Crutzen, J.P. & Mcneill, J. (2008). The Anthropocene: Are Humans Now Overwhelming the Great Forces of Nature. *AMBIO A Journal of the Human Environment*, 36(8), 614. Inapatikana katika https://doi.10.1579/0044-7447(2007)36[614:TAAHNO]2.0.CO;2. Ilisomwa tarehe 12 Juni 2020.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford Press.

TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 3). Nairobi: Oxford University Press.

TUKI (2006). *English-Swahili Dictionary* (Toleo la 3). Mauritius: Book Printing Services.

Waithiru, A.K. (2019). *Matumizi ya Taashira Kuangaza Jiografia na Utandawazi katika Tamthilia za Zilizala na Sudana* (Shahada ya Uzamili, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Laikipia, Nyahururu.

Waithiru, A.K. (2022a). An Evaluation of Environmental Symbolism used in Children Literature: Case Study of *Kijiji cha Ukame* and *Mazingira Maridadi*. *East African Journal of Education Studies*, 5(3), 1-10. Inapatikana katika https://doi.org/10.37284/eajes.5.3.846. Ilisomwa tarehe 1 Machi 2023.

Waithiru, A.K. (2022b). Tathmini ya Binadamu na Mazingira katika Riwaya ya *Nakuruto. Jarida la Mwanga wa Lugha*, 7(2), 163-171.

Waithiru, K.A., Sheila, W.S. & Onyango, O.J. (2023). Tathmini ya Anthropomofiki katika Riwaya ya *Shamba la Wanyama*. *Mulika*, 42(2): 217-237. Inapatikana katika https://doi.org/10.56279/mulika.na42t2.5. Ilisomwa tarehe 21 Mei 2024.

Waithiru, K.A., Wendo, N. & Sheila, P. S. (2024). Kapitalosenia kama Pantoni ya Anthroposenia katika Riwaya ya Kiswahili: Mfano wa *Vipuli vya Figo*, *Mafuta* na *Walenisi*. *Jarida la Mwanga wa Lugha*, 9(1), 91-98.

Walder, D. (2011). *Postcolonial Nostalgias: Writing, Representation, and Memory*. New York: Routledge.

Wallenhorst, N. & Wulf, C. (Wah.). (2023). *Handbook of the Anthropocene Humans between Heritage and Future (Toleo la 1.)*. Switzerland: Springer Publishers.

Watson, N.R. & Watson, R. (2007) *Back to Nature: The Green and the Real in the Late Renaissance*. Pennsylvani: University of Pennsylvania Press.

Yin, K. (2014). *Case Study Research: Design and Methods*. Thousand Oaks: Sage Publications.